TANGAZO LA SERIKALI Na. 539 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA NYANG'HWALE YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 325 la 2022

**1.** Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale ya Mwaka 2024, na zitasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale ya Mwaka 2022 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya jumla

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa-
(a) kufuta maneno "kifungu kidogo cha" na badala yake kuandika "kanuni ndogo ya" popote yanapoonekana katika Sheria Ndogo; na
(b) kufuta maneno "kifungu cha" na badala yake kuandika "kanuni ya" popote yanapoonekana katika Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili la Sheria Ndogo.

Marekebisho katika kanuni ya 8

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 8(7) kwa kufuta maneno "kifungu hiki" na badala yake kuandika "kanuni hii".

Marekebisho katika Jedwali la Kwanza

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kwa-
(a) kufuta kipengele cha 22 katika Sehemu ya III; na
(b) kuongeza Sehemu zifuatazo:

*Tangazo la SerikaliNa.539 (Linaendelea.)*

"SEHEMU YA XIV

Ushuru wa Mazao mchanganyiko

| **Namba** | **Aina ya Zao** | **Kiwango cha Ushuru kwa Shilingi** |
|---|---|---|
| 1 | Viazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | Kabichi | 3% ya bei ya kununulia |
| 3 | Karoti | 3% ya bei ya kununulia |
| 4 | Matunda | 3% ya bei ya kununulia |
| 5 | Vitunguu maji | 3% ya bei ya kununulia |
| 6 | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia |
| 7 | Mchele | 3% ya bei ya kununulia |
| 8 | Mahindi au alizeti au mtama au Mpunga | 3% ya bei ya kununulia |
| 9 | Pamba | 3% ya bei ya kununulia |
| 10. | Zao jingine lolote ambalo halijatajwa | 3% ya bei ya kununulia |
| 11. | Kibali cha kununua mazao | 102,000/= kwa Mwaka mmoja |

SEHEMU YA XV

Ushuru wa Kusafirisha Mchanga wenye Madini

| **Uzito wa Magari** | **Kiwango cha Ushuru (Shilingi)** |
|---|---|
| Ushuru wa kusafirisha mchanga au mawe yenye madini yenye uzito kuanzia kilo 1 hadi 50 kutoka katika eneo la uchimbaji au eneo la leseni kwenda nje ya | 500/= |

| | |
|---|---|
| eneo husika | |

SEHEMU YA XVI

Ushuru wa Karasha na Mwalo

| **Aina ya Huduma** | **Kiwango cha Ushuru (Shilingi)** |
|---|---|
| Ushuru wa karasha au mwalo | 100,000/= kwa mwaka |

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale imewekwa kwenye Sheria Ndogo hii kuzingatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya uliofanyika tarehe 19 mwezi Mei Mwaka 2021 na kuwekwa mbele ya:-

HUSNA TONI CHAMBO
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale

JOHN ISSACK JOHN
Mwenyekiti wa Halmashauri
Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale

NAKUBALI,

Dodoma,
13 Mei, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*